JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

(OR-TAMISEMI)

WAKALA WA BARABARA ZA VIJIJINI NA MIJINI TANZANIA (TARURA)

WAKALA WA BARABARA TANZANIA (TANROADS)

PROGRAM YA MAENDELEO YA BARABARA KWA USHIRIKISHAJI WA JAMII NA UFUNGUAJI WA FURSA ZA KIJAMII NA KIUCHUMI (RISE)

(P164920)

RASIMU YA MPANGO WA USHIRIKISHAJI WADAU (SEP)

JANUARI, 2020

MUHTASARI WA KIUTENDAJI

Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) unahusisha mchakato wa kuwahusisha wadau kwa lengo mahususi la kufikia matokeo ya pamoja. Hivi sasa, Mpango huu unatambuliwa kama mbinu ya msingi ya uwajibikaji kwa kuwa unaitaka asasi kuwahusisha wadau katika kubainisha, kuelewa na kuyashughulikia masuala mahususi ya Programu yanayoibuliwa na wadau kwa ajili ya kutolewa uamuzi, utekelezaji, na hivyo kuboresha utendaji wa mpango/mradi.

Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi unakusudia kuboresha upatikanaji wa barabara ili kusaidia upatikanaji wa kipato kwa watu waishio vijijini, wanaume kwa wanawake, katika maeneo yaliyoteuliwa, na kujenga uwezo wa usimamizi endelevu wa barabara za vijijini kwa kuzipandisha hadhi na kuzikarabati, na pia kutoa msaada endelevu kwa TARURA.

Mpango huu una vipengele vinne (4):

- Kipengele cha 1: Ujenzi na Ukarabati wa Barabara Vijijini
- Kipengele cha 2: Uimarishaji wa Taasisi, Rasilimali Watu na Usimamizi na Ufuatiliaji wa Miradi
- Kipengele cha 3: Uhusihswaji; Ushirikishwaji na Usalama wa Jamii
- Kipengele cha 4: Ushughulikiaji Matukio ya Dharura

Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) utasimamiwa na kutekelezwa na Timu inayoshughulikia Masuala ya Kimazingira na Kijamii ya TARURA/TANROADS. Lengo kuu la SEP ni kufafanua mchakato wa ushirikishaji wa wadau katika Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi, na utoaji wa taarifa na ushauri kwa umma. Aidha, Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) unaorodhesha njia ambazo mawakala watekelezaji (TARURA na TANROADS), wataalamu washauri na wakandarasi watawasiliana na wadau kuhusiana na mbinu zitakazotumiwa kuwaruhusu watu kuibua madukuduku/kero/malalamiko yao na namna yatakavyoshughulikiwa.

Wadau hawa walioainishwa ni wale ambao wameathiriwa na/au vikundi vya wadau wanaopenda kushiriki pamoja na wawakilishi rasmi na wasio rasmi. Utambulishaji wa wadau chini ya Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi utazingatia kazi na majukumu waliyo nayo; na ushawishi/mapenzi yao kwa Programu hii. Watu binafsi ambao wako katika hatari ya kuondolewa kwenye mradi-mdogo ya Programu ya Maendeleo ya Barabara watapewa uangalizi mahususi.

Wadau watakaoshirikishwa katika Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi ni:

- Waathirika chanya – kundi la watu au taasisi ambazo zimeathiriwa na shughuli za ujenzi, kama vile mtu au jumuiya zilizoathiriwa na mradi.
- Waathirikaji hasi – huhusisha watu binafsi au taasisi ambazo zinapenda kujihusisha na ardhi ambayo iko ndani ya eneo la njia (RoW). Wengi wa wadau hawa ni wamiliki wa ardhi zenye majengo tayari au mashamba ambayo yataathiriwa kwa kupoteza ardhi, majengo, na mapato yao ya kiuchumi.
- Vikundi vingine vinavyopenda kujihusisha – kundi la watu au taasisi ambayo inapenda kujihusisha na ujenzi na inaweza kuunga mkono mradi, mamlaka za serikali za mtaa au zile za ngazi ya taifa, wanasiasa katika serikali za mtaa au wa ngazi ya taifa, mamlaka za kijadi, viongozi wa dini, mashirika ya umma yakiwamo yale yasiyo ya kiserikali.
- Watu binafsi waliobainishwa kuwa katika makundi maalumu/ waliopo kwenye hali hatarishi wakiwamo watoto, wanawake, watu wenye ulemavu, wazee na vijana.

Utoaji wa taarifa na ushauri kwa wadau utafanywa kwa kutumia mbinu mbalimbali zikiwamo majadiliano ya vikundi lengwa (kutegemeana na umri, jinsi, na kazi), usaili, watoa taarifa mahususi, na baruapepe. Ushauri utatolewa kwa muda ambao ni utakaowafaa washiriki kwa kuzingatia uelewa wao na pia kwa kutumia lugha ya asili.

Maoni kutoka kwa wadau yatapokelewa na mawakala wanaoshughulikia utekelezaji wa Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi kwa njia ya maandishi na mazungumzo (kwa kutumia sanduku la maoni, viongozi wa serikali za mitaa, mikutano ya hadhara, usaili, n.k.). Timu itapitia maoni ya wadau na kutoa mrejesho wa maamuzi ya mwisho na muhtasari wa jinsi maoni hayo yalivyoshughulikiwa.

Ili kushughulikia malalamiko yanayohusiana na Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi kutoka kwa jamii na umma ulioathirika, Utaratibu wa Kushughulikia Malalamiko (GRM) ulio wazi utaundwa katika Programu hii ambapo kutakuwa na mchakato rasmi wa kupokea, kutathmini na kushughulikia malalamiko hayo. Zitaundwa Kamati za Kushughulikia Malalamiko katika ngazi za Vijiji, Kata, Wilaya, Mikoa, na pia katika Kitengo cha Utekelezaji wa Mradi (PIU) ulio chini ya Programu ya Maendeleo ya Barabara kwa Ushirikishaji wa Jamii na Ufunguaji wa Fursa za Kijamii na Kiuchumi. Kwa wafanyakazi ambao wameajiriwa na wakandarasi, wakandarasi wanaohusika watatakiwa kuandaa utaratibu wa kushughulikia malalamiko kama hitaji la msingi la zabuni.

Waraka wa Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) unaonesha mkakati na mpango wa utekelezaji kwa kuwahusisha wadau tangu mwanzo hadi mwisho wa Programu.

Hata hivyo, Mpango wa Ushirikishaji Wadau (SEP) ndio uti wa mgongo wa mafanikio thabiti na yenye ufanisi. Vilevile, huu ni waraka wa kudumu utakaokuwa ukifanyiwa mapitio na kuboreshwa pale inapohitajika kila mwaka ili kuakisi ushiriki wa wadau kadiri mradi unavyoendelea na wadau wapya watakavyojitokeza.